

SWALI NA. 60

VIBALI KWA AJILI YA KUWEKA MINARA YA MAWASILIANO

MHESHIMIWA SEIF KHAMIS GULAMALI (MANONGA) Atauliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa vibali kwa kampuni ya Halotel na Vodacom kuweka minara yao katika kata ya Igoweko, Uswa, Tambarare, Mwashiku, Ngulu, Ntobo na Mwamala.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Atajibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali Mbunge wa Manonga kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Serikali haina kizuizi kwa Kampuni yoyote inayotoa huduma ya mawasiliano kama itazingatia utaratibu wa kuomba vibali vya ujenzi wa minara yao kwa mujibu wa Sheria pamoja na kupata cheti cha Tathmini ya Mazingira (TAM) kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira (NEMC).

Mheshimiwa Spika, Kata ya Igoweko, Ngulu na Sungwizi zimeainisha na mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na kuingizwa katika orodha ya miradi itakayotekelezwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) ambapo wako katika hatua za mwisho za taratibu za manunuzi ili kuanza kutekeleza miradi hiyo. Miradi hiyo yote inategemewa kukamilika mwezi Aprili, 2019.

Mheshimiwa Spika, Maeneo ya kata za Uswa, Tambarale, Mwashiku, Ntobo na Mwamala zitaingizwa katika orodha ya miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kutekelezwa kutokana na upatikanaji wa fedha.

Hata hivyo, tunatoa wito kwa Makampuni mbalimbali kuendelea kuwekeza minara ya Mawasiliano katika Jimbo la Manonga na maeneo mengine nchini yenye uhitaji kwa kuzingatia taratibu.